

## **TATHMINI YA UGONJWA WA COVID-19 NCHINI KENYA (SEECK)**

### **Utangulizi**

Kadiri janga la COVID-19 linavyozidi kua, ni muhimu kujua kiwango gani cha umma kimeathiriwa na maambukizi, ili kufahamisha maamuzi juu ya chanjo na hatua zingine za kuzuia maambukizi zaidi kama vile “lockdown” ne amri za kutotoka nje, almaarufu, “curfew”. Kabla ya utafiti huu, hatukujua idadi ya watu ambao walikuwa wameambukizwa COVID19 nchini Kenya kwa kuwa hakuna uchunguzi wa kiwango cha idadi ya watu uliokuwa umefanywa. Shirika la APHRC kwa ushirikiano na KEMRI - Wellcome Trust kule Kilifi lilifanya utafiti kukadiria idadi ya watu ambao walikuwa wameambukizwa COVID-19 hapo awali kama inavyothibitishwa na uwepo wa kingamwili (antibodies) dhidi ya SARS-Co V-2 kwenye damu yao.

### **Utafiti huu ulifanywa wapi na lini?**

- Utafiti huu ulifanyika Kilifi, Kisumu na Nairobi kuanzia Januari hadi Mei 2021, kipindi kabla shughuli za chanjo dhidi ya COVID-19 kuwa maarufu nchini
- Kwenye mjadala wa leo, tutazungumzia matokeo ya eneo la Nairobi, haswa, Viwandani/Korogocho

### **Ni akina nani walishiriki Nairobi?**

Wakaazi wa kawaida wa Korogocho/Viwandani katika rika zote walichaguliwa kwa nasibu na kuhusishwa kwenye utafiti huu.

### **Washiriki waliochaguliwa walifanyiwa nini?.**

- Washiriki waliochaguliwa walitembelewa manyumbani kwao na baadaye kualikwa kwenye ofisi za APHRC zilizoko Landmark Plaza/lungalunga plaza kwa mafunzo zaidi
- Washiriki wote walihojiwa ili kuelewa zaidi usuli wao wa kijamii, uchumi na afya
- Milimita mbili za damu zilikusanywa kutoka kwa wale chini ya miaka 5 na milimita tano kutoka kwa wale walio juu ya miaka 5.
- Mpangilio wa kukusanya sampuli za damu katika ofisi za APHRC ulifanywa ukifuata miongozo ya wizara ya afya juu ya kuzuia na kudhibiti COVID-19.

### **Sampuli zilizokusanywa zilifanyiwa nini?**

- Sampuli zilizokusanywa zilipelekwa kwenye mahabara ya KEMRI-CGMRC, zilizoko Kilifi kwa uchambuzi zaidi ili kubaini uwepo wa kinga za mwili (antibodies) dhidi ya virusi vya SAR-CoV2.

### **Matokeo**

#### **a) Idadi ya watu waliokuwa na kingamwili za SARS-CoV-2**

- Tulihoji na kuchukua sampuli za damu kutoka kwa washiriki 869. Kati ya hawa 336 (38.7%) walitoka Korogocho na 533 (61.3%) walitoka katika jamii ya Viwandani.
- Kwa ujumla, karibu wakazi wawili kati ya watano waliopimwa, walikutwa na kingamwili za SARS-Co V-2 (38%).

## Community Engagement Notes for SARs-COV2 HDSS Serological Survey

- Maambukizi yalikuwa chini miongoni mwa miaka 0–10 na kufuatwa na miaka 20 - 29.
- Viwandani ilikuwa na maambukizi ya juu na pia kulingana na miaka isipokuwa miaka 40 - 49 na 50 -59
- Miongoni mwa wakaazi wa maeneo yote mawili, jinsia zote mbili zilithibitisha hatari ya kuambukizwa SARS-CoV-2 (>35%)

### b) Maoni juu ya hatari ya kupata SARS-CoV-2.

- Tuliwaomba washiriki kutathmini hatari yao ya kuambukizwa SARS-Co V-2. Takriban 43% (4 juu ya 10) ya washiriki walio na umri wa miaka 15 na zaidi walihisi kuwa hatari yao ya kupata COVID-19 ilikuwa chini au haikuwepo kabisa.
- Karibu nusu ya wale wote ambao walihisi kwamba uwezekano wa wao kuambukizwa COVID-19 haukuwepo walionyesha kwamba waliwahi ambukizwa awali.
- Idadi hii ilikuwa kubwa zaidi kati ya wanawake kutoka Viwandani ambapo saba kati ya kumi (66.7%) kwa wale walio onyesha kwamba hawana dalili yoyote ya kuambukizwa COVID-19 kwa kweli walikuwa na kingamwili za SAR-CoV-2

### c) Kutoweza kupata huduma za afya

- Tulikagua ufikiaji wa huduma za afya ambazo watu binafsi wangepokea kwa kawaida kabla ya janga la COVID-19. Kwa ujumla, 12. 3% ya waliohojiwa walionyesha kuwa hawakuweza kupata huduma. Kiwango hiki kilikuwa kikubwa zaidi Korogocho (19.4%) ikilinganishwa na 7.9% Viwandani.
- Takriban 27.1% miongoni mwa wale ambao waliripoti kukosa huduma za afya kutokana na COVID-19 walikuwa na kingamwili za SARS-CoV-2 ikilinganishwa na 39.5% kati ya wale ambao hawakukosa huduma.

### d) Kupoteza ajira

- Watu 4 kati ya 10 (40%) ya waliohojiwa walionyesha kuwa wao au mtu fulani nyumbani kwao amepoteza kazi au shughuli za kujimudu kimapato katika muda wa miezi sita iliyopita na idadi kubwa zaidi ikiwa ni wakaazi wa Viwandani ( 41. 1 %) kuliko Korogocho ( 37. 2 %).
- Eneo la Korogocho lilikuwa na kiwango kikubwa cha kingamwili za SARS- COV- 2 kati ya watu kutoka nyumba ambazo wenyeji hawakupoteza ajira (40.8%) ikilinganishwa na (27.1%) ya walioathirika.

### Ujumbe muhimu:

- 1) Maeneo yote mawili (Korogocho/Viwandani) yana hatari ya juu ya maambukizi ya SARS-CoV-2
- 2) Hatari hii ni ya juu zaidi kati ya watu walio na umri wa miaka 10 na zaidi.
- 3) Mtazamo wa hatari ni duni huku watu wengi wakifikiria kuwa hawako hatarini.
- 4) Kuna baadhi ya tofauti kulingana na makaazi ila siyo kwa jinsia
- 5) Maambukizo ya awali haimaanishi kuwa mtu hawezi kuambukizwa tena. Kingamwili hupungua na viwango vinaweza kutokuwa kinga tena.